



USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI



LISHE TANZANIA

Kuboresha lishe ni msingi katika kufanikisha malengo yote ya Maendeleo Endelevu. Uwepo wa utapiamlo sugu (udumavu) unadhoofisha maendeleo katika uhakika wa chakula, uboreshaji wa elimu, na afya bora ya mama na mtoto nchini Tanzania. Lishe duni ndio sababu kubwa ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano nchini Tanzania na inakadiriwa kugharimu serikali asilimia 2.6 ya Pato la Taifa kila mwaka. Upotezaji huu wa mapato uko katika sekta ya kilimo na husababishwa na ukuaji duni wa akili na mwili unaotokana na utapiamlo.

Kulingana na Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya ya mwaka 2015-2016, takriban theluthi ya watoto wote chini ya miaka mitano wana udumavu na asilimia 14 wana upungufu wa uzito. Sababu kuu zinazoongoza kuleta utapiamlo ni ukosefu wa lishe mchanganyiko na bora kwa kila kaya, upatikanaji mbovu wa huduma za afya (pamoja na maji safi na salama, usafi wa mazingira), na mienendo duni ya lishe. Hali ya upungufu wa damu kwa mama ni shida nyingine kubwa nchini Tanzania, ikiwa na asilimia 57 ya wanawake wajawazito na asilimia 46 ya mama wanaonyonyesha wanaathiriwa.

Kama sehemu ya mkakati kamili wa lishe, USAID inazingatia kupunguza kiwango cha udumavu nchini Tanzania kupitia mipango na huduma za afya na kilimo katika ngazi za wilaya na jamii. Uwekezaji muhimu kwenye lishe ni pamoja na: 1) Kuimarisha Taasisi za Serikali za Tanzania na asasi za kijamii (AZAKI) zinazoshughulikia masuala ya lishe; 2) Kuongeza juhudi za mabadiliko ya kijamii na mienendo ili kuboresha namna ya ulishaji wa watoto wachanga na wadogo; na 3) Kuongeza upatikanaji wa lishe yenye afya, lishe mbalimbali kwa mama na watoto. Mradi wa lishe wa USAID unaambatana kabisa na Mpango wa Utekelezaji wa Lishe ya Kitaifa wa Tanzania (2016-2021).

MAELEZO YA LISHE

KIWANGO CHA UFADHILI

- Dola za Marekani milioni 6 kwa

WATEKELEZAJI WAKUU

- Ofisi ya Waziri Mkuu
- Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa Na Serikali za Mitaa.
- Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
- Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania
- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
- Hellen Keller International
- Technoserve

- Save the Children

Mradi wa Lishe unafanya kazi kwa ukaribu na shughuli za minyororo ya thamani ya kilimo

MAENEO YA MRADI

Maeneo husika: Dodoma, Morogoro, Iringa, Rukwa

MAWASILIANO

Janeth Said

jsaid@usaid.gov

Temina Mkumbwa

tmkumbwa@usaid.gov

Grey Saga

gsaga@usaid.gov

MAWASILIANO

Tovuti: www.usaid.gov/tanzania

Facebook: USAIDTanzania

Twitter: @USAIDTanzania

CHANGAMOTO

- Ukosefu wa uhamasishaji kwa umma kuhusu huduma za lishe zinazopatikana.
- Haja ya kuboreshwa kwa sheria na uratibu wa sekta mbalimbali za lishe.
- Vituo vingi vya afya hasa vijijini visivyo na huduma kamili za lishe, na vile vile uhusiano mzuri na jamii wanayoitumikia. Huduma ya afya mara nyingi hupatikana katika umbali mrefu.
- Upungufu wa wafanyakazi wa lishe na wafanyakazi wa afya wenye uwezo wa kutoa huduma za lishe.

MATOKEO

- **Uenezi wa Mradi:** Zaidi ya wanawake milioni 1.6 walio katika umri wa kuwa na watoto na watoto 930,000 walio chini ya umri wa miaka mitano walihudumiwa, kufikia asilimia 97 ya idadi ya watu waliohudumiwa na Feed the Future ya USAID (Dodoma, Iringa, Rukwa na Morogoro). Programu za lishe zinazozingatia afya za USAID pia hufikia maeneo ya Kanda ya Ziwa Pamoja na maeneo ya Mradi wa Ukanda wa Kilimo wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT).
- **Lishe iliyoboreshwa:** Zaidi ya watoto milioni moja chini ya miaka mitano wamepata huduma za lishe.
- **Kupungua kwa Udumavu:** Kunzia mwaka 2011 mpaka 2017, ufadhili wa USAID Katika mikoa mitatu, umechangia kupungua kwa udumavu kwa asilimia kubwa (asilimia 27) miongoni mwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.
- **Mafunzo:** Wataalam wa lishe 22,540 wamepokea mafunzo husika katika kupunguza tatizo la upungufu wa damu na udumavu kwa kwa watoto.
- **Uimarishaji wa Mashirika:** Kujengewa uwezo muhimu kumefanywa kwa AZAKi na Taasisi za serikali kitaifa. Juhudi za lishe zinaunda mtandao wa halmashauri za serikali za mitaa na AZAKi kufikisha jumbe za lishe katika ngazi ya kaya.